




MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na.23. Msimu wa Kilimo 2023/24

Tathmini ya Mei 11-20, 2024 na Matazamo kwa Kipindi cha Mei 21-31, 2024

MUHTASARI

- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo yanayopata mvua za Msimu itasaidia kukomaa na kukauka kwa mazao hususan mahindi na alizeti lakini pia itasaidia shughuli za uvunaji wa mpunga.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara, na Kilimanjaro) inatarajiwa kuathiri ukuaji wa mazao katika maeneo hayo
- Wakulima, wafugaji, na wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao, mifugo na shughuli za uvuvi ili kuweza kukabiliana na athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2024


Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kaskazini na kuwepo katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na magharibi mwa nchi.

Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi lilikuwa la juu ya wastani. Hali hii ilisababisha kutokea kwa mgandamizo mdogowa hewa katika eneo la bahari ambapo katika kipindi hicho ulisababisha kupungua nguvu kwa mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria na magharibi wakati maeneo mengine yalikuwa makavu kwa ujumla.

TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2024

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalipata mvua chini ya milimita (mm) 25. Hata hivyo, maeneo machache yanayozunguka Ziwa Victoria, ukanda wa Pwani ikiwemo kisiwa cha Pemba ambayo yalipata mvua kiasi cha mm 51 hadi 150. Aidha, maeneo mengi ya kanda ya kati, magharibi na nyanda za juu kusini magharibi yalikuwa makavu kwa ujumla kama inavyoonekana kwenye Kielelezo.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa siku kumi kwa kipindi cha Mei 11-20, 2024

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2024

Katika dikadi hii, mvua zilizonyesha katika maeneo machache zilisaidia ukuaji na maendeleo ya mazao.

Maeneo yanayopata mvua za Masika, mahindi yapo katika hatua ya kukua isipokuwa katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria ambako mahindi yapo katika hatua ya kukomaa.

Katika maeneo yanayopata mvua za Msimu, mahindi yapo katika hatua ya kukomaa.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya kukomaa na kukauka hususan kwa maeneo ya mikoa ya Rukwa, Tabora, Mbeya, Shinyanga, Mwanza na Morogoro na wakulima waliendelea na uvunaji wa zao hilo.

Zao la alizeti lipo hatua ya kukomaa katika mikoa ya Singida na Dodoma, na wakulima walikuwa wanavuna zao hilo wakati katika mkoa wa Morogoro zao hilo lipo hatua ya kutoa maua.

Maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama yalikuwa ya kutosha katika maeneo mengi nchini.

**HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA
MEI 11-20, 2024**

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mabonde hakikuwa na mabadiliko makubwa katika maeneo mengi nchini.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA
KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2024**

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kuwepo katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria.

Joto la bahari katika eneo la mashariki na magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu katika kuimarisha mifumo isababishayo mvua. Kwa upande mwingine, uwepo wa kimbunga "IALY" unatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani hasa katika kipindi cha mwanzoni mwa dekad.

**HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA MEI 21-31, 2024,**

Maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na mikoa ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba) pamoja pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) inatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara, na Kilimanjaro) pamoja na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) zinatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) zinatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

**HALI YA HEWA KILIMO:
MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI
CHA MEI 21-31, 2024**

Mvua zinazotarajiwa kunyesha katika maeneo machache hususan katika maeneo yanayopata mvua za masika zitasaidia ukuaji na maendeleo ya mazao.

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika mikoa ya kanda ya kati (Dodoma na Singida), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) itasaidia kukomaa na kukauka kwa mazao hususan mahindi na alizeti lakini pia itasaidia shughuli za uvunaji wa mpunga.

Hata hivyo, hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara, na Kilimanjaro) inatarajiwa kuathiri ukuaji wa mazao katika maeneo hayo.

Kwa ujumla, wakulima wanashauriwa kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali ya hewa inayotarajiwa, milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza huku wakipata ushauri kutoka kwa maafisa kilimo katika maeneo yao.

Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na Maziwa Makuu ili kufanya maamuzi ya wakati muafaka wa kwenda kuvua kuepuka athari za upepo mkali.

Wafugaji wanashauriwa kuhifadhi majani ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya baadae.

**HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA MEI 21-31, 2024**

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mita hususan kwenye maeneo ya pwani vinatarajiwa kutokuwa na mabadiliko makubwa.